

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

Simu: +255262963309/13/14
Nukushi: +255 262 963 316
Barua pepe: ps@lands.go.tz
Tovuti: www.lands.go.tz



*Mji wa Serikali, Mtumba,
S. L. P. 2908,
40477 DODOMA.*

TAARIFA KWA UMMA

UTARATIBU NA NJIA YA ULIPAJI WA KODI YA PANGO LA ARDHI

Ardhi yote ya Tanzania ni ya umma, hivyo, raia yoyote wa Tanzania anayo haki ya kukalia na kutumia ardhi kwa mujibu wa Sera na Sheria za ardhi. Haki hiyo inatoa masharti mbalimbali kwa wamiliki wa ardhi miongoni mwake ikiwa ni sharti la kulipa Kodi ya Pango la Ardhi. Malipo ya kodi yanayotozwa kwa wamiliki wa ardhi kutokana na fursa wanayopata ya kupangishwa ardhi ambayo ni ya umma.

Kila mmiliki wa ardhi amepewa sharti la kulipa Kodi ya Pango la Ardhi kwa kila mwaka kwa mujibu wa **Fungu la 33 (1) la Sheria ya Ardhi (Sura ya 113)**.

Utaratibu na Njia ya Ulipaji wa Kodi ya Pango la Ardhi

Malipo ya Kodi ya Pango la Ardhi hufanyika kwa kuzingatia ukubwa wa ardhi inayomilikishwa, matumizi ya ardhi yaliyoidhinishwa, thamani ya ardhi na kiwango cha malipo ya mbele (premium) ya ardhi inayomilikishwa. Ulipaji wa Kodi ya Pango la Ardhi hutolewa kupitia ankara ya malipo ambayo itakuwa na namba ya kumbukumbu kwa ajili ya malipo (**control number**). Wamiliki wa ardhi wanaweza kupata makadirio pamoja na ankara ya malipo kwa utaratibu ufuatao:-

- (a) Upokeaji wa ankara za malipo kupitia vituo vya makusanyo ambavyo ni; Ofisi za ardhi za Mikoa na Ofisi za ardhi katika Halmashauri zote nchini.
- (b) Ukadiriaji wa Kodi ya Pango la Ardhi kwa kutumia simu ya kiganjani kwa kupiga Na. ***152*00#** menyu kuu ya malipo ya Serikali sehemu ya kukadiria kodi ya kiwanja.

(c) Ukadiriaji wa Kodi ya Pango la Ardhi kupitia tovuti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. www.lands.go.tz, kupitia ukurasa wa huduma kwa mtandao kisha sehemu ya kadiria kodi ya ardhi.

(d) Upokeaji wa ankara ya malipo kupitia mawasiliano yanoweza kufanyika baina ya mmiliki wa ardhi na watoa huduma kutoka Kituo cha Huduma kwa Wateja cha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupitia mawasiliano simu ya kiganjani **0739 646 885** au simu ya mezani **026 216 1610**.

Baada ya kupata makadirio ya kodi, unaweza kulipa kupitia;

(a) Benki au mawakala wa benki wa NMB, CRDB, NBC, TPB au AZANIA Benki; au

(b) Kwa njia ya simu ya kiganjani kwa kufuata taratibu za miamala ya malipo ya Serikali kupitia simu.

Naomba pia nitoe ufafanuzi juu ya mkanganyiko ambao umekuwa ukijitokeza kwa wananchi kuhusu utofauti uliopo baina ya Kodi ya Pango la Ardhi (Land Rent) na Kodi ya Majengo (Property tax). Kodi ya Pango la Ardhi kama nilivyoeleza hapo awali, hutozwa kwa wamiliki wa ardhi tofauti na Kodi ya Majengo ambayo hutozwa kwenye majengo/nyumba. Aidha, kodi ya majengo imewekewa utaratibu wa ulipaji na ukusanyaji wake ambapo kwa sasa inalipwa kwa njia ya malipo ya ununuaji wa umeme kupitia mfumo wa LUKU.

Naomba kuisitiza kwa wamiliki wote wa ardhi nchini, kutekeleza sharti la kulipa kodi ya ardhi kwa kuwa sasa tumeboresha njia za ukadiriaji na ulipaji wa kodi husika kidigitari. Aidha, niwakumbushe maelekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wakati wa kuhitimisha Hotuba ya Bajeti 2024 Bungeni, Wizara imedhamiria kuchukua hatua kwa wamiliki wote wa ardhi watakaoshindwa kutimizi masharti ikiwemo kuwafikisha mahakamani ili kuuza mali zao kufidia kodi ya ardhi na kupendekeza ubatilisho wa milki zao.


Geophrey Mizengo Pinda (Mb.)

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI